**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA FEDHA

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA UNUNUZI WA UMMA**

PPRA
Public Procurement Regulatory Authority

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na: CA.192/211/01/B/8** **23 Septemba, 2024**

Kwa Taasisi Nunuzi Zote,
**Tanzania Bara.**

Yah: **WARAKA WA MABADILIKO YA KANUNI Na. 167 KUHUSU MATUMIZI YA RASILIMALI ZA NDANI KATIKA KUTEKELEZA MIRADI YA UJENZI**

Tafadhali rejeeni kichwa cha habari hapo juu na Kanuni Na. 167 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 iliyoelekeza matumizi ya rasilimali za ndani (force account) katika kutekeleza miradi ya ujenzi.

2. Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) inapenda kuzijulisha Taasisi nunuzi zote nchini kuwa, Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 817 la Septemba, 2024, imefanya marekebisho katika kanuni ya 167 (2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 kwa kuongeza ukomo wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa kutumia utaratibu wa *force account* kutoka shilingi milioni mia moja (100,000,000) hadi shilingi milioni mia tano (500,000,000). Kwa mujibu wa kanuni hii, matumizi ya utaratibu huu wa force account ni pale tu ambapo taasisi nunuzi itakuwa ikitekeleza mradi wa ujenzi kwa kutumia watumishi na vifaa vyake au kwa kushirikiana na fundi au taasisi nyingine ya umma.

3. Kwa mujibu wa Kifungu cha 76 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka, 2023 na kanuni ya 167 ya Tangazo la Serikali Na. 518 ya Mwaka 2024 kama zilivyofanyiwa marekebisho kupitia Tangazo la Serikali Na. 817 la Mwaka 2024, taasisi nunuzi zinaruhusiwa kutekeleza miradi ya ujenzi kwa utaratibu wa *force account* endapo:

a) kazi za ujenzi zitakazotekelezwa ni ndogo, zimetawanyika na zipo katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi kiasi kwamba makandarasi wenye sifa hawawezi kushiriki na kufanya kazi kwa bei nafuu;

Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma

b) kazi za ujenzi zinatakiwa kutekelezwa bila kuvuruga utekelezaji wa shughuli za taasisi zinazoendelea;

c) kutakuwa na muingiliano wa shughuli za taasisi usioepukika na ni vema kwa kazi za ujenzi kutekelezwa na taasisi yenyewe au mamlaka ya umma kuliko kutekelezwa na mkandarasi ili kupunguza hatari;

d) kuna dharura inayohitaji utatuzi wa haraka;

e) taasisi nunuzi ina wafanyakazi wenye sifa na vifaa vya kusimamia na kutekeleza kazi za ujenzi zinazohitajika;

f) matengenezo au ujenzi ni sehemu ya shughuli za kawaida za kila siku za taasisi nunuzi husika; na

g) thamani ya ujenzi iliyokadiriwa haivuki kiasi cha shilingi milioni mia tano.

4. Aidha, endapo thamani ya ujenzi iliyokadiriwa **inavuka shilingi milioni mia tano**, mradi husika unaweza kutekelezwa kwa utaratibu wa *force account* baada ya **Afisa Masuuli wa taasisi nunuzi kutoa idhini ya kutumika kwa utaratibu huo**. Idhini hiyo itatolewa kwa mujibu wa kanuni ya 167 (3) ya Tangazo la Serikali Na. 518 ya Mwaka 2024 kama zilivyofanyiwa marekebisho na Tangazo la Serikali Na. 817 la Mwaka 2024, baada ya kufanya yafuatayo:

a) kutathmini hitaji la utekelezaji wa kazi za ujenzi husika kwa kutumia utaratibu wa *force account;*

b) kuhakikisha uwepo wa watumishi wa umma wenye sifa za kusimamia ujenzi husika kwa mujibu wa mwongozo utakaotolewa na Mamlaka;

c) kuhakikisha uwepo wa mafundi wenye sifa stahiki kwa kuzingatia aina ya kazi ya ujenzi katika mradi husika; na

d) kufanya tathmini ya gharama na muda wa utekelezaji wa mradi kwa kutumia utaratibu wa *force account* ikilinganishwa na matumizi ya njia zingine za utekelezaji wa kazi za ujenzi.";

5. Taasisi nunuzi zinataarifiwa kuwa kwa mujibu wa kanuni ya 167A ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 kama zilivyofanyiwa marekebisho na Tangazo la Serikali Na. 817 la Mwaka 2024, katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa utaratibu wa *force account* Afisa Masuuli anatakiwa kuwasilisha kwa Mamlaka-

Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma

(a) taarifa ya kuanza kazi za ujenzi kwa kutumia rasilimali za ndani ndani ya siku saba baada ya kuanza ujenzi; na

(b) taarifa za utekelezaji wa kazi za ujenzi uliokwishakamilika kwa kila awamu ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kukamilika kwa kazi za ujenzi husika.

6. Endapo kazi za ujenzi zimetekelezwa kwa utaratibu wa *force account*, Mamlaka itafanya ukaguzi maalum wa thamani ya fedha ili kujiridhisha kuhusu hitaji la matumizi ya utaratibu wa *force account* katika kazi za ujenzi husika, thamani halisi ya fedha ya bidhaa na huduma zilizotumika na muda wa ujenzi husika. Iwapo baada ya ukaguzi Mamlaka itabaini kuwa taratibu za matumizi ya *force account* zimekiukwa na taasisi nunuzi, Mamlaka itapendekeza kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali au chombo kingine chenye mamlaka hatua stahiki za kuchukuliwa dhidi ya afisa masuuli wa taasisi nunuzi husika.

7. Taasisi nunuzi zinakumbushwa kuwa, ununuzi wa bidhaa au huduma zitakazotumika kama malighafi katika utekelezaji wa miradi utazingatia masharti ya Sheria na Kanuni za ununuzi wa umma. Aidha, Taasisi nunuzi zinatakiwa kuteua msimamizi wa mradi mwenye sifa zilizotolewa na kutambulika na Bodi husika za kitaaluma.

8. Pamoja na maelezo ya Waraka huu, taasisi nunuzi zinatakiwa pia kuzingatia Mwongozo wa Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi kwa Utaratibu wa Rasilimali za Ndani (Force Account) uliotolewa na Mamlaka.

Waraka huu umetolewa na:

Dennis K. Simba
**MKURUGENZI MKUU**